Halafu tunakuja katika familia tunasema kwamba mtu yeyote yuko na haki ya kuwa na familia ikiwa umefikisha miaka 18 na umekubaliana na mwenzako uko na haki ya nyinyi kuungana na kuanzisha familia yenu. Tunasema pia nchi hii yetu ya Kenya itasisitisa sana madili ya familia yaweze kuangaliwa sana yaweze kupewa kibao mbele ili tusije kupata maadili ya kigeni ambayo hayahusiani na madili ya kiafrica ambapo Kiafrica tunasema familia yiko mbele hapo hatutaki maadili ya kigeni ambayo itakuja kutatiza maisha ya familia zetu.

Tunasema ya kwamba watu wote ambao wako na vilema watapewa haki zao na tutaangalia na tutahakikisha katika jamii zetu kwamba watu hawa wanaangaliwa na haki zao zote zinaangaliwa. Tunasema kwamba kila mwananchi atakuwa na haki ya kuishi na furaha na kuheshimika kwamba hakuna mtu yeyote ambayo hatakufungia wewe heshima yako kama mwananchi ama heshima yako wewe kama binadamu.

Na tunasema hivi, tunasema ya kwamba mwananchi atakuwa na uhuru wa yeye kupata kuangaliwa yaani uhuru wa kulindwa. Uhuru wa kulindwa tunamaani kwamba tuko na Jeshi letu litatulinda sisi kama Wakenya tuko na polisi watatulinda sisi kama raia, tuna uhuru huo. Na wakati ambapo kama mimi nikitoa mfano katika mji yetu huu tunakaa tunakuta tuko na wezi wengi, tunasalilishwa tuko na uhuru sisi wakuinuka na kusema Katiba inasema kwamba tuko na uhuru wa kulindwa, je ambao wanafaa kukulinda wako wapi? Kwa hivyo tunapewa uhuru wa kuuliza ulinzi wetu.

Halafu tunasema kwamba tuko na uhuru sisi ya kutokufanywa watumwa ama kulazimishwa na mtu yeyote kufanyishwa kazi. Tunasema pia ya kwamba tuko na uhuru wa sisi kujifanyia mambo yetu ubinafsi, tuko na uhuru wa usiri wetu. Ukitaka wewe kukaa nyumbani kwako ufanye mambo yako kwa siri, uko na uhuru huo. Mtu yeyote hana uhuru wa kuja kuingia nyumbani kwako kuuliza ni nini unafanya ndani ya nyumba yako? Uko na uhuru wa kujifanyia mambo yako wewe mwenyewe na

kunyamaza na mambo yako. Isipokuwa tu mambo haya isiweze kuwa kwamba yanatafusiana na maadili ya nchi yetu.

Halafu tunasema kwamba mtu yeyote ana uhuru wa kuabudu chochote ambacho anachotaka yeye wenyewe, ana uhuru wa kujiunga na dini yoyote ana uhuru wa kuwa na imani yeyote ile ambayo anapenda kuwa nayo yeye mwenyewe. Tunasema kwamba mtu yeyote mwananchi ana uhuru wa kujieleza, unaweza kukaa ukiamini ya kwamba hivi ni sawa na hivi si sawa, nchi yetu inasema ya kwamba utakuwa na uhuru wa kujieleza kwa njia yeyote ile. Tunasema kwamba pia kutakuwa na uhuru wa mtu kusema unavyotaka. Hivi sasa labda wengine tuko katika maisha yale ya samani tunaogopa, nikisema hivi labda wenzangu wataona shida. Mtu atakuwa na uhuru wa kusema na kujieleza na kusema chochote anachotaka hata kama itakuwa yeye yuko upande ule mwingine kwamba anasema mambo ambayo wenzake hawangeyapenda. Ila katika kusema haya tunasema, kwamba utayasema yale unataka kusema lakini hutaleta gazia kwa njia yeyote ambayo utakayokuwa umeyasema.

Tunasema kwamba kutakuwa na uwezekano wa mambo yote ambayo ungetaka kujua utakuwa na uhuru wa kuuliza mambo haya yako wapi. Utakuwa na uhuru wa kupata habari zozote. Tukisema uhuru wakupata habari ni kwamba utakuwa na uhuru wa kusikiliza shirika lolote la habari zile unataka kusikiliza utakuwa na uhuru wa kusoma gazeti lolote, na kama kuna mambo pia yako katika Serikali ambayo ungetaka kujua una uhuru wa kwenda kule na kuuliza kwamba upewe habari zile.

Tunasema tutakuwa na uhuru wa kuchangamana yaani tutakuwa na uhuru wa sisi kama tulivyo kaa hapa, tunaweza kuitana sisi kama wananchi tukaweka vikao vietu tukakaa tukazungumzia masalaha yetu bila mtu yeyote kuja hapa kutusumbua ama kututenganisha. Pia utakuwa na uhuru wa sisi kutoka nje na kujieleza yaani demonstration. Tutakuwa na uhuru huo kwamba tunaweza kutoka nje tukaakilisha masalaha yetu kwa wananchi wenzetu.

Tutakuwa pia na uhuru wa siasi kwamba mtu yeyote anaweza kujiunga na chama chochote cha kisiasa ambacho angependa, mtu yeyote pia angekuwa na uhuru wa kuweza kufanya siasi aina yeyote ile ambayo angetaka. Tutakuwa na uhuru pia wa kuwa na makao kwamba Serikali ina jukumu ya kutupa sisi makao, nafikiri wakaaji wa Majengo swala hili mnalielewa saidi. Serikali itakuwa na jukumu ya kuwapa nyinyi kama riaia wa Kenya makao na mtakuwa pia na uwezo wa kuishi sehemu yeyote katika nchi hii. Utaweza kuhama hapa uende uishi Kisumu, utaweza kuhama hapa uende kuishi Mandera, bila mwananchi yeyote upande ule kukueleza kwamba wewesi mkaaji wa hapo. Unaweza kuishi sehemu yeyote katika nchi yetu ya Kenya.

Kutakuwa pia na uhuru wa wakimbizi nafikiria wengi wetu tunaolewa tatizo la wakimbizi lile tuko nalo nchini pia hao wakimbizi wako na haki zao na wako na uhuru wao kiasi fulani, kwa hivyo wao pia watakuwa na uhuru wao.

Tunasema ya kwamba tutakuwa na uhuru wa watu kuweza kufanya biashara na watu kuweza kufanya kazi zozote zile ambazo wao wenyewe wangependa kuzifanya. Kazi yote utafanya kutafuta riziki yako utakuwa na uhuru wa kufanya

Tutakuwa pia na uhuru wa mtu kuwa na mali yake nakuweza kujifadhia mali yake ila mali hii tu iwe inapatikana kwa halali.

Isewe tena mali hii umemnyang'anya mwananchi mwenzako.

Halafu tunasema kwamba kutakuwa na uhuru wa wafanyi kazi. Wafanyi kazi watakuwa na uhuru wa kulipwa mshahara unaofaa. Watakuwa na uhuru wa kufanya kazi katika sehemu ambazo ni sawa wao kufanya kazi ambapo masilahi yako ya kikazi yanaangaliwa vizuri, watakuwa na uhuru wa kugoma. Na pia wenye kuwaajiri watakuwa wanawapa wafanyi kazi wao uhuru wa kuweza kulingania mambo yote ambayo yatausia na uwaajiri wao. Tutakuwa na uhuru wa sisi kuitisha haki zetu za afya. Nafikiria wengi wetu mnaona Serikali yetu ina matatizo kwa hivyo tutakuwa sisi na uhuru na haki ya kuuliza kuhusu afya zetu.

Tutakuwa na uhuru pia kuusia na elimu. Hapa tunazungumzia kwamba tunasema elimu ya shule za msingi iwe ni lazima. Narudia tena, elimu ya msingi iwe ni lazima na iwe ni bure. Kwanza itakuwa ni bure halafu na itakuwa pia ni lazima. Kwa hivyo utaweza wewe kama mzazi kukaa nyumbani na mtoto, itakulazimu wewe umpeleke shule, na tunasema hii elimu ya msingi ambao ni ya chini kabisa iwe bure kabisa, usiseme kama mzazi nimeitishwa hiki wala hiki. Mtoto asome bure.

Tunasema kwamba tutakuwa na haki za kuweza kupata nyumba na Serikali itashugulika kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata makao. Pia utakuwa wewe kama mwananchi, utakuwa na uhuru na haki ya kupata chakula chako cha kila siku. Kwa hivyo Serikali itahakikisha kuwa nchi imekuwa na usalama kiasi cha kwamba wewe kama mwananchi unaweza kuendelea na shuguli zako za kutafuta riziki yako ya kila siku. Tutakuwa pia na haki ya kuweza kupata maji nafikiria Serikali wakati mwingi imetueleza kwamba baada ya labda mwaka wa 2010, inatazamia kuwa kutakuwa na mfereji wa maji mmoja kwa kila watu kumi katika nchi. Kwa hivyo una haki ya wewe kupata maji safi. Pia kutakuwa na haki ya wewe kuishi katika mazingara masafi, mazingara yatakuwa na vyoo na shughuli zingine ambazo zinahusiana na haya. Wengi wetu tumesikia watu wakilalamika miti inakatwa, kwa hivyo utakuwa na haki juu ya mazingara yako.

Tunasema pia utakuwa na haki kuhusian na lugha yako na mila zako utaweza kuwa na haki ya wewe kuzungumza lugha yako ambayo unaipenda na pia utakuwa na haki ya wewe kufanya mila zako ambazo unazipenda. Ila pia tunasema mila hizi sizije zikatofautiana na miadili ya nchi yetu ya Kenya. Labda nikiguzia kama mila moja, kuna mila hizi wengine wanafanya za Kutahiri wanawake. Mila kama hizo hazitakubalika kwa kuwa zitakuwa zinahitilafiana na miadili ya nchi yetu ya Kenya na Katiba yetu. Kwa hivyo ikiwa mila zako hazijamuudhi mtu yeyote ama hazijahitilafiana na Katiba hii yetu ya sasa, itakuwa ni sawa, ukiamua mila yako labda inasema uimbe barabarani ni sawa kabisa utakuwa na haki hiyo.

Tunasema kwamba wewe utakuwa, wewe uko na haki kama mnunuzi. Wengi wetu labda hawajajua kwamba wao kama wanunuzi wako na haki. Uko na haki ukienda dukani, kitu chochote ambacho unanunua lazima kiwe kimefikia standards ambazo zimewekwa na nchi hii. Ukienda kununua sabuni kama ile sabuni, kama imeandikwa inatoa pofu nyinyi, uko na haki wewe ukinunua ile sabuni ikutolee ile pofu, ikiwa hiyo sabuni haitatoa hiyo pofu uko na haki ya wewe kama mwananchi kulalamika na mambo mengineo.. Kwa hivyo wewe kama mnunuzi uko na haki juu ya kitu chochote ambacho utakachokinunua

kwamba kitakuwa kimefikia zile standards ambazo wao wenyewe wanasema. Ukinunu gari ikiwa wamesema hili gari linaweza kutembea ndani ya maji, likikosa kutembea ndani ya maji uko na haki kama mwananchi kuuliza.

Tunasema kwamba pia tutakuwa na haki ya sisi kuongozwa kwa uadilifu kwamba viongozi wetu ambao tutakuwa nao watatuongoza sisi kwa uhaki. Pia tuko na haki ya sisi kama raia kukataa, mambo yoyote ama sheria zozote ambazo sitakuwa hazina uhaki ndani yake. Ikiwa mtu yeyote atataka kutuongoza kwa sheria ambazo hazina uhaki ndani yake sisi kama wananchi tuko na haki yakukataa. Tunasema tutakuwa na haki ya sisi kuweza kufika makortini na korti kusikiliza malalamiko yetu na kutusikizia kesi zetu.

Watu ambao watakuwa labda kwa njia yeyote ile wamemeshikwa na polisi, wakawa kama sasa wao ni wafungwa pia watakuwa na haki zao ambazo ziko zinaandikwa kwa urefu. Mtu yeyote ambao ni mfungwa atakuwa na haki ya yeye kupata wakili kama hana uwezo wakupata wakili Serikali itahakikisha kwamba mtu huyu amepatiwa wakili wakumsimamia katika masalaha yake kortini.

Tunasema pia kutakuwa na haki ya mtu yeyote kuweza kufanyiwa kesi yake kwa uhaki na kwa uadilifu na ikiwa kesi hii ataona haikufanywa kwa usawa ana haki ya yeye kutuma rambi rambi zake na pia kuna sehemu tunaitengeneza ambapo wananchi wote wanaweza kupeleka malalamiko yao kuhusiana na Serikali.

Tunasema kwamba watu ambao watakuwa wamefiliwa labda mtu yeyote ambaye amefungwa atakuwa na haki zake na moja wapo kama hizi haki, ikiwa amefungwa muda mudogo atakuwa yeye yuko na haki zake za kupiga kurua na haki zingine ambazo zimeelezwa hapa kwa urefu.

Tunasema kwamba mwananchi yeyote atakuwa anaweza wakati wowote kurudi katika haki za kibinadamu kuziangalia na akiona kwamba haki zozote zake za kibinadamu hazijaangaliwa kwa uzuri yuko na haki ya kushtaki na kuuliza haki zake za kibinadamu.

Halafu mwisho tutakuwa na sehemu ambayo tunaipangia kuita Commission of Human Rights and Administration of Justice. Yaani katika hii Katiba mpya tunasema kwamba tutaanzisha kikindu ambacho kitashugulikia masalaha ya haki za binadamu na uongozi wa sheria. Sasa katika sehemu hii sisi kama wananchi tutakuwa na uwezo na haki ya sisi kutoka kwenda kulalamikia haki zetu za kibinadamu ambazo zitakuwa zimedharauliwa, ambazo tutakuwa tumenyimwa ama haki zingine ambazo tutakuwa tunahizi ya kwamba tumenyang'anywa.

Halafu tunasema kwamba korti zetu zitakuwa zimepewa jukumu la kuhakikisha kwamba haki za kibinadamu zimefuatwa. Tunasema kwamba korti zetu zitakuwa zimepewa jukumu la kukaa na kueleze wananchi kuhusu haki zao za kibinadamu na vipi haki hizi zinahusiana na sheria.

Nafikiria kama mtu yeyote ana swali tumeulizwa kwamba maswali yote tuyaandike chini halafu baadaye, mtakuja mtuulize maswali yenu halafu yatajibiwa. Asante.

**Eunice Kamau :** Tunasema ya kwamba ni vizuri tukiandika maswali yetu chini, kusikie ndio baadaye tutauliza maswali. Kuna kitu ningependa sasa kuwauliza ndio tujue kwa ajili ya masaa. Kama tungeendelea na Kizungu peke yaka ama mngependelea Kizungu na Kiswahili pia. Kiswahili peke yake kuna wengine wako na tatizo ya Kiswahili peke yake. Kuna mtu ako na shida yeyote na Kingereza? Mngependa ikorogwe pamoja? Tuchanganye?

**Interjection from the floor :** (inaudible)

**Eunice Kamau :** Ile shida iliyoko ni ya kwamba wale walioko na jukumu ya kupatikana hii dissemination, wanasikia wako nyumbani wakiongea Kingereza. Haya basi nitawauliza wajaribu.

Haya sasa ile sehemu ingine ama sura ya sita ni mimi nitaongeza, mimi nitaongea kile kiswahili cha mama Njeri. Sitafanya Suleiman afafanue nitafafanua wenyewe.

Katika Katiba yetu mpya ukianagalia ukurasa wa kumi na moja hiyo ndio iko ile sura ya sita nitaongea. Na katika hiyo sura iko na sehemu tatu. Ya kwanza ni mambo ya uchaguzi na kupiga kura, ile nyingine ni Tume ya uchaguzi. Ile nyingine ni juu ya vyama za kisiasa. Kwa hivyo katika hizo sehemu tatu, inapatia wananchi vile watakuwa wakihuzika katika kutawala nchi yetu. Na kwa hivyo tutasikiliza kwa makini sana ndio tujue ni vipi wewe ukiwa mwananchi wa Kenya utakuwa ukihuzika na uongozi wa nchi. Ni vipi utahusika?

Ya kwanza juu ya kupiga kura na uchaguzi Katiba mpya inasema ya kwamba kila mwananchi wowote ako na haki ya kupiga kura, na kila mwananchi ako na haki kama amefikisha miaka. Ako na haki ya kusimama kuchaguliwa kiti chochote cha kisiasa anapendelea kuchaguliwa. Na katika upigaji kura, upigaji kura utakuwa kwa TV, na utakuwa free and fair na pia katika uchaguzi kutakuwa na kina mama. Hii ni mara ya kwanza kina mama wamepatiwa sehemu kubwa kwa hivyo wakati huu katika uchaguzi ni lazima kina mama watakuwa wakisimama, si sasa wanaume peke yao. Hata kina mama watakuwa na haki ya kusimama. Na pia vilema, mara ya kwanza wamepatia sehemu yao. If there is anybody who is disabled, they are free to stand to be elected. Na pia Bunge litaamua, ama litapitisha sheria juu ya number ya, tutakuwa na Constituencies ngapi, na katika provincial council, district council, local council na village council. Kwa hivyo Bunge litatoa sheria juu ya vile Constituencies sitakuwa. Na pia itatoa sheria juu ya nomination of candidates, kwa hivyo, haitakuwa tu vile political party wanataka, hapana, Bunge litaamua sheria ndio kuwe kukijulikana watu watachaguliwa vipi.

Tena Vyama vya kisiasa – Vyama vyote vitahakikisha ya kwamba sehemu tatu ya wale watu wanasimama a third of the people

to be elected are women at least a third of its candidate for direct election will be women. Na vile pia tumesema juu ya disabled watakuwa na nafasi yao.

Na juu ya kupiga kura tuone vile Katiba inasema juu ya kupiga kura. Mtu yeyote akifikisha umri wakupiga kura ako na jukumu ya kupiga kura. Na ni nani atapiga kura, but ni nani ako na ile jukumu ya kupiga kura. Mtu yeyote akiwa na miaka kumi na nane, mtu akifika miaka 18 amekjubaliwa kujiandikisha kuchukua kura yake. Na nilisikia juu ya mtu akiwa mwananchi wa Kenya pia kuna patiano ni vipi kuhusu yule amejandikisha kuwa a Kenyan citizen ni vipi anaweza pia kuchukua kura katika sehemu ya B na ile ingine. Na ni nani anaweza kukatazwa kujiandikisha? Kama mtu, if one is not of sound mind tuseme kama mtu ni mwenda wazimu, ama ako na shida tofauti, tofauti, vile sina hakika kwamba mtu hawezi akajiandikisha, hiyo inabidi mtu asije akajiandikisha. Pia kama mtu akipatikana, na hapa ni muhimu sana msikilize, kama mtu akijulikana ya kwamba amekuwa akitenda kitendo kibaya wakati wa uchaguzi, Bunge linaweza kupitisha sheria likasema huyo asije akisimama, ama akajiandikisha. Ile nyingine ni ya kwamba, kwa ajili ni Katiba, Bunge pia litapitisha sheria juu ya mambo ya, kama mtu amesuililiwa kujiandikisha, unaweza ukaenda kortini ukajitetea ndio uonyesha sababu ile ujakubaliwa kujiandikisha.

Ile nyingine ni juu ya unopposed candidate, kama mtu akisimama, amesimamishwa na chama fulani na hakuna mtu hata mmoja anampinga hii Katiba mpya inasema huwezi kwanda bila uchaguzi wowote, ni mpaka kuwe na voting ndio ihakikishwe ya kwamba fulani alichaguliwa na kura elfu ngapi mpaka watu waende wakapige kura ndio ujulikana, hata kama hukupingwa na mtu yoyote, ulikuwa na kura ngapi.

Ile nyingine ni juu ya Tume ya uchaguzi. Katika hii sura ya sita kuna sehemu ya Tume ya Uchaguzi na inasema ya kwamba kutakuwako na Tume ya Uchaguzi. Naye Tume ya Uchaguzi, kutakuwa na mwenye kiti na katika hiyo Tume ya Uchaguzi watakuwa watu kutoka wanane na kumi huwezi ukaenda chini ya watu nane na juu ya watu kumi. Ile nyingine ni ya kwamba mwenyekiti wa Tume mpaka achaguliwe na Bunge. Bunge likikusanyika bunge ndio litakuwa na jukumu ya kujua mwenye kiti ni nani. Haitakuwa tu fulani, fulani ndio mwenye kiti ya Tume, lakini Bunge litakuwa na jukumu la kuchaguiwa mwenyekiti wa Tume la Uchaguzi.

Ile nyingine ni ya kwamba mtu kama amesimamia ungozi fulani tuseme umechaguliwa kama Mbunge ama una jukumu fulani katika public office huwezi ukawa wa Tume ya Uchaguzi. You cannot hold a public office, neither can you be a member of Parliament. So if you want to be a member of Electoral Commission, then one should not be nominated from either of those sectors. **(end of side B tape 1)**

Tume ya Uchaguzi inaweza kukata kuandikisha chama chochote kama ikijulikana ya kwamba hicho chama kinaleta mambo ya dini, ama hicho chama kinaleta mambo ya ukabila. Na hayo yote mnaona katika hiyo sehemu ya pili A na pia chama chochote hakitakiwi kupigana ama kufurukisha watu kwa kupigana na ya kwamba Tume ya Uchaguzi itakuwa ikitakikana kuweka account zao vizuri, kwa hivyo wakikusanya pesa ama wakipatiwa pesa na Tume ya Uchaguzi, wanatakikana kuweka account

zao vizuri na hizo account zao zitakuwa, all their accounts will be checked. All their accounts will be supervised and they will be checked and within three months to the end of the financial year, they are supposed to submit their financial accounts. Ile nyingine ni kwamba Tume ya Uchaguzi inaweza ikafutulia mbali chama chochote cha kisiasa wakipatikana wanajihusisha na mambo machafu, vile nilifafanua hapo mbeleni.. Ile nyingine ni ya kwamba Chama ya Uchaguzi itakuwa kwa wakati wa kwanza ikipatiwa fedha wakati wa siasi ama chama chochote kikihundwa kitakuwa kikipatiwa pesa na Serikali ama na Tume ya Uchaguzi ili, to propagate its own political vision, during the election time and also to run its own office affairs. Na pia itakuwa ikikubaliwa kuchukuwa pesa kutoka kwa wananchi. Ile nyingine ni ya kwamba Rais wa Kenya ama mtu yeyote ule ako na public office hakubaliwe na Katiba mpya kuwa na office yeyote katika chama, in the political party. The President or any public official or the deputy secretary in the new Constitution, those persons are not allowed to hold any political office. So I have tried to run over the three chapters. I am sure you have read them.

Na wakati huu tutaendelea katika sura ya saba na nane na nitamualika Lwanga aje apatiane.

**Lwanga Tabu :** Mimi nitaongea kwa lugha ya Kingereza kwa sababu Kiswahili yangu ni mbaya. Kwa jina naitwa Lwanga, District Coordinator, Kamukunji/Makadara. I will tackle the Legislature, the Executive and Devolution of power. Nitaanza na Legislature.

Parliament shall consist of the National Council and the National Assembly. The National Assembly shall have 210 Constituency MPs and 90 Party list MPs. These are MPs who will be elected from the list provided by political parties. The National Council shall have 70 members and these 70 members will come from each district plus 30 women members who will come from the provinces.

The Role of Parliament – The following will be the role of the Parliament. Enacting legislation and consulting on promolocation of regulations, providing a national forum for deliberation on and dissolution of issues of concern to the people, approving expenditure of the State and appropriating funds as required to meet those expenditures. Considering and passing amendments to the Constitution as provided for in Chapter 18. Scrutinizing and overseeing actions of National government: Considering and approving international treaties. Confirming the President’s choice of person to serve in the Cabinet. Advising on and consenting to appointment to be made by the President as required by the Constitution for legislation, bulabulabula. You can see, that is contained in Article 102 Chapter 7 page 13. Approval of appointments by Parliament that is Article 103. Appointments in respect of the following institutions shall be referred to the National Council for approval before they are made:

- (A) Judicial Service Commissions
- (B) Ethics and Integrity Commission
- (C) National Land Commission
- (D) National Environmental Management Commission

(E) Teachers Service Commission

(F) Salaries and Remuneration Commission

Please check on Article 103 you will see all those things I have pointed out.

Appointment in respect of the following offices shall be referred to the National Assembly for approval before they are made:

(A) Prime Minister

(B) Deputy Prime Minister

(C) Ministers

(D) Deputy Ministers

(E) Permanent Secretary

(F) Ambassadors and High Commissioners

(G) Electoral Commission

(H) Auditor General

(I) Controller of Budget

(J) Director of Central Bureau of Statistics

(K) Governor of Central Bank

I will go to Article 108, it deals with qualifications and disqualification of members. A person is eligible to be a member of Parliament if that person is

(A) a citizen of Kenya

(B) has attained the age of 35 years in the case of National Council

(C) has attained the age of 21 years in the case of the National Assembly

(D) is qualified to vote for an election for Parliament

(E) has attained at least Form 4 standard of education with a pass and he is proficient in Kiswahili and in English but persons who only express themselves in sign language are qualified.

(F) Satisfy any moral and ethical requirement verified by the Constitution or an Act of Parliament.

You can read that in your own time.

Under the Draft Constitution the electorate will be empowered to recall a member of Parliament who does not perform. Check Article 112 Clause 1. Subject to this Article the electorate for any constituency has the right to recall their member of Parliament before expiry of the term of Parliament. A members referred to in Clause 1 may be recalled from that office on any of the following grounds :

(A) Physical or mental incapacity rendering that member incapable of performing the functions of the office or

(B) Misconduct likely to bring hatred, ridicule, contempt or disrepute to the office

(C) Persistent desertion of the electorate without reasonable cause.



I will go to the Executive, that is Article 149 – The National Executive of the Republic of Kenya comprises, the President, the Vice President and the Cabinet appointed under Article 151.

The authority of the President that is Article 150. The President is the Head of State, Commander in Chief of the Defense Forces, these are what we used to call Armed Forces, the Chairperson of the National Security Council and the Chairperson of the Defence Council. He is a symbol of the unity of the Nation and has responsibility to promote and enhance the unity of the Nation. Safeguard the sovereignty of the Republic, promote respect, diversity of the people and protect their human rights and fundamental freedom. Shall uphold, safeguard and respect the Constitution and the rule of law.

State functions of the President Article 151. The Presidents shall address the opening of each newly elected Parliament in accordance with Article 141.

**Interjection from the floor :** (inaudible)

I will summarize and then we give you an opportunity to raise issues that you have. I was on the State functions of the President:

- (A) shall address the opening of each newly elected Parliament in accordance with Article 141
- (B) shall address a special sitting of Parliament once each year as provided for in Article 14
- (C) May address Parliament at any other time and
- (D) May dissolve Parliament only in the circumstances contemplated at Article 142

That is all I had as far as the Executive is concerned you can read in your own time, I will go to Devolution of power.

Devolution of Power is Chapter 10

**Interjection from the floor :** (inaudible)

**Lwanga Tabu :** I will stop there and the audience can raise the issues they have, thank you very much.

**Eunice Kamau :** Asante sana, mnajua juu ya Katiba ni haki ya mwananchi na yule mwananchi ameongea ni kweli tangu asubuhi mmekeki hapa na tutaendelea na hiki kikao cha kupatikana juu ya Katiba kwa wale hawawezi wakasoma hii Katiba mpya lakini wakati huu tutapatia nafasi mtu yeyote vile tuliambiwa mkumbuke tumekuwa na vikao viwili hapa katika Constituency yetu tukipatiana mawaidha na recommendation zetu juu ya Katiba mpya. Imekuja mko na vile vitabu mbele yenu na kwa hivyo kama kuna kitu chochote ulikisoma unasikia ah, ah, ah! Hii sikubaliani nayo ni vizuri kuongea. Na kama kuna kitu chochote ukiongea na labda umesikiliza ama umesoma ukajua ya kwamba haikuandikwa ni wakati huu wakupatiana, na vile

tuliambiwa na Esther asubuhi mukumbuke ya kwamba sisi tukiwa katika hiki kikao hatuna uwezo wa kubadilisha, yetu ni kupatikana maoni. Na wakati wa kubadilisha utafika. Na kwa hivyo nivizuri mukipatiana maoni yenu kama mmefurahia semeni mumefurahia, kama hajafurahia uko huru kusema kitu chochote kile ungetaka kusema juu ya Katiba mpya. Kwa hivyo wakati huu tutakuwa tukiongea juu ya katibe mpya. Tunaelewana hapo. Okay. Na mnajua ukipatikana kila kitu kitakuwa recorded ndio mtu asije akasema apana na kama kuna kitu haijsemwa tuliambiwa recommendations sote za Kamukunji ziko hata mkitaka kuziona uende kwa office ya Lwanga. Na wakati ule unauliza swali kwa ajili tuko wengi tufupishe maswali yetu. Niliwaambia muandike. Kama unataka kuuliza swali kama kuna mahali huelewi vizuri ama kuna recommenation ama kuna ile unataka itolewe, chukua dakika tatu jukumu ni lako sasa. Karibuni wananchi.

Kwa hivyo tungechukua majina ya wale wangependa kwanza kuja ndio kama una kitu ungependelea utakuja hapa ndio uongeshe wananchi uwaambie vile ungependa kwa hivyo ningeliza Esther. Kuna mama mmoja hapa chukuwa jina lake. Nani mwingine angependa. Chukuwa huyu mama kwanza, chukuwa ule baba pale, ule kijana, na wa nne hapa. Mama njoo hapa ujiandikishe pale vile nimesema ndio tutaita majina vile itakuja. Tafadhali wale wengine wakiendelea wale wanatake kuuliza ama kupatikana mapendekezo yao jiandikishe pale ndio twende upesi.

**Amina Bakari :** Nataka kusema, polisi ananyanyaza watu, akikuta ananyang'anya mfuko anatoa pesa watu wako na shida. Anaenda kupiga ugali huko na bibi yake. Ukimwitia mwizi hawezi kumshika. Sisi hatuna kazi, tuko na tabu. Tuko na tabu, sisi hatuna kazi, tunaonewa, sisi ni maskini ya Mungu tunaweza kwenda kwa Bunge tunatafuta kazi, sisi hatuna kazi, tunaenda maofisini tunatafuta kazi. Wengine hupewa kazi wakubwa kwa wakubwa. Barabara zijengwe. Takataka zizolewe. Tuone wakubwa. Tusidharauliwe hata siku moja. Chakula zipunguzwe bei. Kuna maskini kuna tajiri. Maskini tunaonewa, tuna haki gani sisi.

**Eunice Kamau :** Haya asante mama. Ibrahim Mohamed?

**Ibrahim Mohamed :** Mimi ningependa kusema katika National Holidays, National days.

Katika kifungo cha National days, kuna Madaraka Day, Jamhuri Day na Constitutional Day. Lakini kama vile hii Review Commission imeheadiwa na Religious organizaitona, hatuoni kam Idd Day hivi ya Waislamu. These days kwa nini mmesikata off. Tunaona mumetu-deny right yetu hapo. Na ingine ni katika registration of political parties, the same ina-apply mume-cut off, religious parties mnasema religion isiwe involved, where hii Constitutional Review is driven, iko na power ya religious organizatios, kwa hivyo hapo naona mtakuwa mumetu-deny right yetu. Kwamba hatuwezi ku-vote on religious basis, mnataka tu-vote katika which basis? To register katika satanic basis ama which basis mnataka. Kingine ni katika human dignity, hatujui hii body itakuwa inaongezwa na watu gani kwa sababu tukipatia Serikali wa dignify kuhusu mtu na si-specialist, ambao kuna mambo ya kumi kumi pombe pia ina-lower down dignity ya mtu, miraa the same. Kwa hivyo hii body, hiyo Act ni ndogo sana ingekuwa, iko supposed to be addressed which specialist atai-check. Another thing in katika mambo ya arrest. Hatuoni kama Police Station ndio zimekuwa handicapped enough kwa sababu unaweza remain 48 hours katika custody. Imagine two days

uko police station mambo mangapi yatakuwa yamekupita. At least Police station pia zingekuwa handicapped kama inge-establish independent days ukishikwa na police badala ya kuingizwa custody iwe watu independent waangalie kama hii crime imetendeka kwa sababu 48 hours kwa mtu mwenye shuguli zake ni ages. Zangu tu ni hizo.

**Eunice Kamau** : Haya asante sana. Ule mwingine ni Abdul

**Abdul Isadeko** : Nafurahi sana kupata nafasi hii ya kuzungumza maoni yangu kidogo kuhusiana na Katiba hii ambayo ni ya Yash Pal Ghai pamoja na Makamishna, tunawashukuru kwa kututengeneza Katiba ya nchi hii na tunafurahi na tunaunga mkono wote ambao wamahusika kutengeneza Katiba ya nchi hii ya Kenya na sisi jambo lile nilikuwa nazungumzia ni kwamb kuna maswala kama ya uhuru wa kujieleza, freedom of religion believe and opinion. Sasa katika jambo kama hilo, this Article is not specific on matter of sexual expression e.g. homosexuality, child pornography, lesbianism and other immoral acts as championed by the Western nations. Kwa hivyo lile jambo linahusu kila mtu tunaweza kusema tunapatia watu freedom, lakini freedom ya ku-express each and everybody's personal views and expression, inaweza kuwa misused katika kutangaza hali za homosexuality, maana yake ukienda katika Western Countries, utaona homosexuality ina right katika ile Katiba ya nchi ile. Kwa vile hapa kwetu, itakuwa namna gani? Tukisema kwamba tusiwe very strong against it, itaingizwa katika Katiba na itawezekana kama lesbians na homosexuality itakubalika katika nchi hii.

Jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kuzungumzia linahusiana na, kuna institutions zingine ambazo zina-adapt forcefully, prayers za asubuhi in one religion. Na hiyo is not fair tukisema kwamba prayers sitakuwako asubuhi kwa watoto wetu wasali katika dini zote, ama kama sivyo hiyo prayer itolewe kabisa watu waendeleo bila kama hizo katika nchi za makaribi prayers hakuna hii ni ku- instill watoto katika mambo ambayo ni ya religion na kuwafanya kuwa na tofauti ambazo si nzuri.

Jambo lingine ni kuhusu malipo ya uzeeni ama ambayo imewekwa katika Katiba ya sasa kwamba kila mwananchi atapewa benefits na Social Security, tulikuwa tunataka kujua kama huwo mswada utapitika katika Bunge wakati gani, na ilo jambo litahusu pia wale watu ambao walikuwa hawajafanya kazi mbeleni ama itakuwa namna gani.

Na pia jambo lingine ni la manyumba. Nauliza hakuna Clause yeyote has been put to the effect of the provision of housing as to whether we should take housing to include shanties na manyumba mabox. Serikali inaweza kukamilisha hili jambo vipi? Itapata pesa wapi ya kujengea kila mtu nyumba? Tusifurahi tu na hatujui pesa zitoka wapi za kujengea watu manyumba? Shantis, sinakubaliwa kama ni nyumba? Tafadhali tupate maelezo.

Halafu land and property ownership. Kuna watu wengine umejipatia land kubwa sana katika Kenya. Mtu ambaye amekuwa katika office ya urais ama ofisi za uwezo katika nchi hii wamechugua land titles kubwa sana na sehemu kubwa ya nchi kwa wenyewe peke yao. Unapta mtu ako na acre 5,000, 10,000 hata 20,000. Alipataje hizo? Ama ni kupewa alipewa. Basi tueleze. Kwa sababu watu wengi hawana mashamba na hizo shamba zikawanywe, watu wapate shamba.

Halafu mambo ya Judiciary. Ningependa kujua kwamba Commission ama Sheria itachukua hatua gani kwa hawa maakimu wawili ambao wamejaribu kufuruka Constitution? Sisi tunapinga kabisa jambo kama hilo. Tunaona kwamba huu ni utofu wa nidhamu. Na kufikiria mambo ya ulafi, tumbo lako unalifikiria vipi. Hao majaji wameonyesha kuwa hawana sifa za kuweza kwendelea katika hali ya kuwa ni majaji wa nchi hii.

Citizenship ya nchi hii – watu ambao wameendelea kuishi katika nchi ya Kenya, kuanzia independence mpaka wakati huu wazamehewe na amnesty saa hizi na wapewe uwezo wa kupata kitambulisho pamoja na uraia wa Kenya bila kusumbuliwa. Ni hayo tu.

**Eunice Kamau :** Asante sana wale wameandika memorandum zao please mziwaje hapa ni vizuri tukipatiana ziende kule mbele. Beatrice Kinuthia.

**Teresia Kinuthia :** Asante sana lakini ninaitwa Teresia Kinuthia na vitu viwili tu niliona ningetaka kuchangia. Ya kwamba vyama vya kisiasa vitakuwa vikipewa pesa za kuendesha shuguli zake. Hata ingawa the intention is good watu wengi wanaweza kupata majaribio ya kufungua vyama vya kunufaisha wao wenyewe. So that can be scrutinized more carefully so that, tusiwe na vyama ambavyo vina hundwa kwa kujifaidi wenyewe.

The other one is election of party members, usha chaguliwa na uko kwa Bunge na tuliambiwa unaweza kuitwa na watu. Recalling of MPs. The MPs opponent can start using the community, so that you will be called back, kwa sababu ulimshinda. So those are reasons that should be taken care of. Tusiwe na watu wa aina hiyo. Asante.

**Eunice Kamau :** Beatrice Njeu. Jackson ulikuwa hapa, hapana. Jackson K. Muguu

**Jackson Muguu :** Yangu ni madogo saidi sana. Nilikuwa nataka kujulisha kiongozi wetu walio Pumwani hapa nashukuru kwanza mbele ya Makamishna ambao tuko nao hapa. Kwa sababu ile kitendo wanafanya iliongelewa na Mzee Jomo Kenyatta, na nilikuwa ninataka, pengine nilikuwako wakati huo niongeee ile maneno kidogo. Ninakumbuka ya kwamba kutoka 1963 Mzee Kenyatta akienda kupewa madaraka, Madaraka Day anaulizwa na British hao ni Wazungu wa ng'ambo. Mzee Kenyatta ndio tutaenda kukupa madaraka na tutakupa Jamhuri Day, je utatengeneza Katiba yako ambayo itakayolinda nchi hii yetu? Akasema mimi sitatengeza Katiba kwa sababu sina wasomi ambao wakujua Katiba ni nini, nitaendelea na Katiba yenu mpaka nifikie miaka 25. Nataka kujulisha nyinyi kweli Katiba yetu ndio hii inaundwa lakini mjue kuna kitu moja tunadai Wazungu walienda nayo. Walakini Mzee Jomo Kenyatta, Mzee mheshimiwa aliposema hivyo aliandamishwa kidogo, na Wazungu walisema kama ni sheria yetu ndio utaendelea nayo hapa Kenya basi na mali yetu iko hapa sisi ----- British, tutachukuwa Title Deed ya Kenya kwa sababu tungali tunalinda Kenya. Mkae mkijua hiyo kitu bado tunadai deni yetu.

Ya pili walivyo ondoka kwenda kupewa Jamhuri na Madaraka day wakaenda ng'ambo, mjue kuna kitu mbili ambayo mko nayo hapa. Jamhuri Day ndio hii na mjue nchi hii ikipigana na wazungu walikuwa wakipigania haki yao. Sasa walipoondoka walijukua ile barua yao wakaenda nayo Title Deed yetu ya Kenya walipo kwenda nayo. Hadi ni deni kwa hivyo sisi tunashukuru Makamishna wakati huu walikuja kutukundulia, kuchapa, kutengeneza Katiba ya kulinda nchi yetu ya Kenya. Je Katiba hii itafuatana kwenda ng'ambo ituitishie Title Deed yetu kwasababu ndiyo mali yetu ya Kenya hii na ndio tulikuwa tukipigania. Ya pili ndugu zangu nieleze nyinyi, wanachuoni wetu na wanaounda Katiba hii waende ng'ambo watuletea Title Deed yetu. Shukrani ndugu zangu na dada zetu.

**Eunice Kamau :** Yule mwingine nitamwita ni Hezron Sambu.

**Hezron Sambu :** Ninafurahi sana kwa watu wa Tume ya Katiba, nilishangaa sana kwa mtu yetu moja akisema sisi yiko nja na sisi na nja hii ambaye itakwenda paka watoto wetu mpaka tukufe mpaka kila kitu. Hata kulala bila njaa na hi kitu inafanywa usiku na mchana. Kitu ambaye nafikiri sitasoma ni uchaguzi ya chief. Uchaguzi ya chief siku hizi inaletwa ile askari ambaye ameiba amefanya nini ametoroka anakuja kuletwa pahali hapo. Huyu ni chief, na wewe uwezi kujua. Mimi nasema shauri ya reserve si hata hapa Pumwani, unaona kesho, unaona watu wanapigwa, na kwenda kwa pombe watu wanauwana. Tafadhali chief aletwe halafu vile nimeona ni raia wajionee. Kama zamani huyo chief hata kama ni assistant chief yote ni sawa hata kama ni mama ameletwa, kimombo siku hizi inakuja, hata kama ni mzee yeyote yote inajulikana.

Ya pili, waheshimiwe wenye kupata taabu sana kwa kutengeneza mambo hii yetu, ni wagonjwa, wagonjwa unaona mtu amekuwa mgonjwa sana anakwenda Kenyatta unaona anawanjwa hapo – hakuna pesa - unaona akilala tafadhali muingilie hapo sana kwa sababu watu wengine kama hapana mpa kitu kidogo hawa madakitari watawacha. Hiyo ni kitu ambayo imekuwa kubwa sana.

Ya tatu ni upande wa land, mashamba siku hizi. Mashamba tulifurahi sana kwa President alipovunja maneno ya korti halafu, mashamba yaangaliwe na village. Sababu kama mtoto amezaliwa hapo, hakuna mwingine ambaye anakuja na kunyang'anya hiyo shamba. Hata kama hapa Pumwani unaweza kuona mtu anakuja tu ananunua nyumba na kununua nyumba hajui ile mtoto amezaliwa mama ameolewa hapo mzee huyu ameo hapo anakuja kufukuza na kuanza mambo yake kama biashara tafadhali sana kwa sababu shamba na nyumba yote yiko pamoja. Tumepate taabu hata saidi hapa kwa hivyo iangaliwe na villagers na kadhalika.

Nimeona Katiba kidogo ambayo inaandikwa, sisi tunataka customary law. Customary law ni kitu ambaye Mungu alifanya watu. Kama alifanya ni mtu fulani watu wa Coast anaimba vile ilivyo anaona raha vile ilivyo kama wanandi wanaimba kame kikuyu wanaimba, lakini si ya kuwa tunagawanya. Customary laws kuna saa, saa ile ya arusi au kitu fulani, msinyime watu vile wanafanya customary laws. Hata kama vile siku ya arusi kuna vitu ambavyo watu wanafanya. Kuna watu wengine kama kule wakuria au pande ingine, watu sasa wanaanza kufanya watoto watahiri hata kidogo wakificha. Sisi tunataka mama

ameshamzika mtoto mkubwa aulizwe kama anataka shauri yake, kama hataki si kwa lazima. Hiyo kitu itapotea peke yake. Nafikiri ni hayo tu, siwezi kuzungumza mengi. Lakini sana hatutaki nyumba unaona watu siku hizi watu wanakuja wazee ya mji au chief anasema kata hapa kwa hivyo anahuza kesho unakuja amefukuzwa.

**Eunice Kamau :** Okay, asante sana baba. Yule mwingine ni Ruth Nasiyo.

**Ruth Nasiyo :** Asante sana kwa Kamishna wetu wale wameakilisha hii Katiba kuja hapa siku leo kupokea maoni na pia kutuletea yale ambayo tulizungumza. Mimi yale nitazungumzia leo, ni kwa upande ya Presidential Escort. Nitazungumzia mahali pa sensitive area. Wakati wa Rais, kuna wakati mwingi sana tunapoteza pesa kila wakati Rais akienda Airport wakina mama kwa DO pesa nyingi sana kutoka kwa PC zinatolewa huko kwa PC kwa DO magari zinawekwa akina mama kwenda Airport kumsindikiza President akienda safari. Tena kila wakati akitoka safari hao mama ama watoto wa shule pia wanaambiwa watu watoke kwa shule wasimame nje ya barabara ili wakimngojea President akitoka safari na kila wakati President huwa anaenda official duty kwa nini hata watu wa biashara wanasimamishwa wasifanye biashara sababu President anakuja na huyu President ameandikwa mshahara ako kwa kazi yake ambaye inamlipa mshahara. Tunataka wakati President ako na official duties, kama ana mgeni rasmi kutoka nje anakuja kututembelea ndio hiyo .pesa ziwe zinatoka kwenda kulaki huyo mgeni. Kama kwako nyumbani mgeni akija utakuwa prepared hata watoto wako utawambia leo tuna mgeni anakuja tuwe tayari ku-welcome mgeni si wewe kila wakati ukitoka pesa zinatumika ati unazindikiza President. Tena watu wanawacha kazi. Hiyo yote ni kama kuangusha nchi kwa sababu hata economy yetu inaendelea ikififia sababu ya vitu ndogo ndogo kama hizo. Sababu hizo zinaharibu nchi, hizo pesa zingefunguliwa hata project, hiyo project ingepatia hata kijana wetu kama hawa kazi ambaye wangejiendeleza nayo. Kwa hivyo mwangalie sana upande wa matumishi ya pesa. Hii kutumia pesa ya uma ovyo, ovyo ndio imefanya watu hawawezi kuwa na maendeleo ya kifedha sababu ya mtu mmoja kuwa anatumikia pesa, spending too much money on one person at the expense of others. Hiyo ndio kitu ambaye nimezungumzia hapa na ningependa sana muende hii maneno makapeleke huko mbele sababu tunaharibu uchumi. Tunapeleka President, tunamtoa, tunampeleka, na hakuna special duty is ambayo tunaenda kufanya. **(end of side A tape 2)**

**Eunice Kamau :** Yule mwingine ni Abdulahi.

**Abdulahi Ramadhani :** Sina mengi ya kuzungumza, yangu nitataja tu baadhi ya vipendekezo zangu. Ya kwanza ni kuwa President yule, in the office of the President tunamwona bado akiwa na power nyingi zaidi to an extend that kila mtu anakuwa na matumaini ya kuwa President. Kila mtu ukimwona anataka kuwa President. Ile kitu iko inatakiwa hizi powers ziwe trimmed. We have graduates, university students, lecturers who are jobless, these opportunities sikiwa divided equally to all those students, hii economy tunaweza ku-revive. Si kazi mia moja inapatiwa mtu moja Nia moja inapatiwa mtu mmoja while elfu kumi wameketi bila kazi.

Ya pili – Pendekezo yangu ilikuwa ni about retirement benefits. I think each and everybody tunaangalia under President mtu

anaona hata ni heri awe President for one second halafu aitische retirement ili apata those benefits.

Ya tatu is still under the current Constitution. I don't see where wamezungumza about the freedom fights to honour the heroes of Kenya. There is nowhere they have talked about these people who played a key role for us the coming generation, I want to see the current Constitution to ensure that our grant parents who are still here or those who died for our country, they are being honoured and being recognized very well for the role they played for this nation.

The other thing that I want to talk about, I think the Constitution, this is a fundamental issue whereby we should not just look at it as a paper it is a document which will govern us for more than 100 decades to come so, I think this is the kind of Constitution we need but still we need to go through it. There is no need for us to rush it because of politics because of this short time. And this is an important document that will govern Kenya for another 100 years to come. The issue is that let Constitution continue until we come up with a good constitution which will manage to govern this country for another 100 years without any other problem. And also the kind of reviewing of our economy. We have all over people spending billions of shillings because they want to become President now but let me tell you my people. Who ever will become President there is no way he will help you. It is high time for Kenya to realize that they are the ones who can be able to recover the economy by hard working and trying to elect genuine leaders. There is no way mtu anatoka tu huko anakuja kwetu, mimi nataka mbunge wetu. Hiyo wakati imekwisha. Siasa ya unga na sukari nataka iishe.

**Eunic Kamau :** Abdullahi kama una point ingine ongea ingene wacha.

**Abdullahi Ramadhani :** Last but not least, I want to say thank you to the Commissioners and let us hope a peaceful nation, let us pray to God to give us a wise, a genuine, a leader with medeocracy and integrity for our nation thank you.

**Eunice Kamau :** Okay thank you very much. Please come and sign the book. The other person is Samuel Karanja.

**Samuel Karanja :** Hamjambo nyote, mimi nasema ya kwamba sababu hii muda wa kusoma hii Katiba na kujibu hiyo maswali inaonekana ni muda mfupi sana. Na kama mimi ni mwalimu tunawale tunafunza na hao tukagua hii Katiba kwa muda usiyosidi mieze miwili. Muda usiyozidi miezi miwili. Sababu kuna mahali ingine tuliandika kitu ingine inaitwa Kenya Development Plan kuhusu mashamba na hiyo nimesoma plan sikuiona mahali popote. Tulisema mtu awe na acre 1000 mtu aliye na shamba kubwa saidi. Ekari tano, tano igawiwe wananchi wasio na chochote na kuhusu Katiba hii sababu ni maoni ya wananchi wa Jamhuri hii yetu Kenya, imekubalika moja kwa moja na ithinishwe na kongomano la kikatiba na Bunge vile, vile ithinishwe na nani anatawala aweke sign na tuendeleo na uchaguzi chini ya Katiba mpya. Sina saidi ya hiyo asante.

**Eunice Kamau :** Thank you very much. Next



**Emmanuel Mtinda :** Thank you very much for the good work that you are doing. I think the Review Commission has done a very good work it has produced a very good document and we are really supporting you for that. So my first recommendation is that Ministers should be chosen from the MPs. Because most of the people are ambitious to get to Parliament so that they can be awarded these positions. So it is very good for us to choose Ministers among the MPs. Because of attracting professionals. Secondly I don't support the idea of having two Houses because the National Assembly can do the duties of the National Council. Secondly there has to be a distinction between public holidays and National holidays because we don't know where things like Christmas falls in. Another thing is that we should document the customary laws because most of them are actually verbal. So most of us may be in Nairobi we don't understand what customary law says and most of the time we find that they preach the Constitution of the land. Another thing is that the President should not have powers to remove the Auditor General without the consent of the National Assembly. My views were just those. Thank you.

**Eunice Kamau :** Thank you. Next

**Mohamed Ramadhani :** Mimi yangu ni machache kwa ajili ya identity card. Tunapata taabu sana kwa kupata hizi vipande zetu. Tukienda huko kuchukuwa vipande uanaambiwa leta form ya kuzaliwa ya mtoto wetu. Tukienda tunaketi kwa committee huko. Ikipitishwa huko tunawekewa watu hata huwajui ni watu gani, na DO yuko hapo na wazee wengine wanawekwa hapa. Sasa ikishapitishwa huko, ikienda huko juu tena ikirudi inaletewa vikwazo vingine tena, unaambiwa wewe ni mtu wa Mijikenda huwezi kupata hii. Sasa hiyo tutafanyaje kwa watoto wetu hawa wazidi kupata vipande? Maana yake hata sasa nina msichana wangu mmoja amezaliwa hapa, hapa maternity hata barua yake ninayo hapa, nikienda kuuliza habari ya hicho kipande wanasema huwezi kupata kwa jili unaandika wewe ni Mijikenda. Na huyo Mijikenda si Mkenya? Na ndio kabila Mijikenda. Mimi sina mengi ila ni hayo tu.

**Eunice Kamau :** Next

**Mark Musila :** Okay asanteni sana mimi ningependa kusema mambo machache kuhusu Constitution. The security of the common man. The security of the common man haijakuwa classified kwa hiyo mambo ya Constitutional review kwa sababu tukiangalia wale watu ambao wako na security properly ni wale watu wakubwa. Lakini sisi watu wachache, especially mimi hata nikitoka hapa nikitembea, nikifika hapo nje, haki zetu zinakuwa abused by the Administration. Kwa mfano unaweza patwa hapa na ushikwe na uanze kupigwa search. Na uambiwe wewe ulipatikana ukiwa umelewa na in common sense wewe ulikuwa unatoka kazini umechelewa unaenda nyumbani unapata the Administration wame-abuse haki zetu wananchi kwa wakati mrefu sana. Sasa sijui hii Constitutional Review itafanyake kuhusu hii mambo ya kushikwa kwa njia halafu unaenda unapewa accusation ile ambayo hujui.

